

# Imarisha Azimio Lako: Ubikira

Biblia inasema: “Mjiepushe na uasherati.” (1 Wathesalonike 4:3) Imarisha azimio lako na ujihakikishie kwamba utafaidika ukitii sheria ya Mungu kwa kuwazia jinsi mambo yanavyoweza kuwa.





Je, sheria ya Mungu ina vizuizi vikali?

Kwa nini Mungu anawakataza watu ambao hawajafunga ndoa wasifanye jambo ambalo linafurahisha?

Fikiria hali zifuatazo . . .

HALI YA 1
## HISIA

HALI YA 2
## KUSHINIKIZWA

HALI YA 3
## NAFASI

HALI YA 4
## MATOKEO MABAYA

Vijana wengi ambao hufanya ngono kabla ya ndoa hujuta baadaye. **Unafikiri ni kwa sababu gani?**

________________________________

________________________________

Karibia wasichana wote wangependa mvulana ambaye *atawalinda,* siyo ambaye atawatumia. Na wavulana wengi hawavutiwi na msichana ambaye akitongozwa anakubali kufanya ngono. **Unafikiri ni kwa sababu gani?**

________________________________

________________________________



www.jw.org/sw © 2016 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

# ELEZA

Jibu maswali yafuatayo.



## HALI YA 1 HISIA

Kwa nini hisia za ngono hazipaswi kuonwa kuwa "adui"?—**Soma Methali 5:18, 19.**

Je, hisia za ngono ndiyo hisia pekee zenye nguvu unazopata? (Taja baadhi ya hisia nyingine.)

Je, unatenda mara moja kila wakati unapopata msisimko wa ngono? NDIYO HAPANA

Je, unaamini kwamba unaweza kudhibiti hisia zako za ngono? NDIYO HAPANA

Kwa kuwa Mungu aliyeumba hisia za ngono, anasema pia ujifunze kujidhibiti, hilo linaonyesha ana uhakika gani na wewe?—**Soma 1 Wathesalonike 4:4.**

## HALI YA 2 KUSHINIKIZWA

Kwa nini unafikiri baadhi ya watu huwadhihaki mabikira?

Kwa nini huenda wenzako wakakushinikiza ufanye ngono?

Unapaswa kuwaonaje wale wanaokushinikiza uvunje amri ya Mungu?—**Soma Methali 13:20.**





## HALI YA 3 NAFASI

Unapaswa kuepuka watu, sehemu, na hali gani ili usishawishike kufanya ngono kabla ya kufunga ndoa?



www.jw.org/sw © 2016 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

HALI YA 4

## MATOKEO



Si rahisi kwa watu wenye mwenendo mpotovu kingono kubadili tabia zao kwa sababu wamefunga ndoa. Jambo hilo linaonyeshaje umuhimu wa kuepuka kufanya ngono ukiwa mseja?—**Soma Wagalatia 6:7, 8.**

---

Unafikiri kuna faida gani ya kubaki bikira hadi wakati wa kufunga ndoa?

---

Je, unaamini kabisa kwamba kutii sheria ya Mungu ya kuepuka uasherati kutakupa furaha zaidi kuliko kufuata maisha ya "uhuru" wanayoishi vijana wenzako? Ikiwa ndivyo, kwa nini?

---

# WEKA MIKAKATI

HALI YA 1—HISIA
Ikiwa ninashawishika kufanya ngono, nitafanya mambo yafuatayo:

---

HALI YA 2—KUSHINIKIZWA
Vijana wenzangu wakinidhihaki kwa sababu ya ubikira wangu au wakinishinikiza nifanye ngono, nitasema hivi:

---

HALI YA 3-NAFASI
Nikiwa katika hali inayoweza kuniruhusu nifanye ngono, nitafanya mambo yafuatayo:

---

# UNAWEZA KUFANIKIWA!

Ukiimarisha imani yako sasa, utafanya uamuzi mzuri, hata wakati unaposhinikizwa!



www.jw.org/sw © 2016 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania